## TUME YA TAIFA YA UMWAGILIAJI

## TANGAZO MUHIMU KWA WAKULIMA WA SKIMU ZA UMWAGILIAJI NCHINI

Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inawakumbusha wakulima katika Skimu za Umwagiliaji kote nchini, kulipa Ada ya Huduma za Umwagiliaji kabla ya kuanza kwa shughuli za kilimo kwa msimu ujao.

Malipo ya Ada ya Huduma za Umwagiliaji ni utekelezaji wa Sheria Namba 4 ya mwaka 2013 (Sura 435), kifungu cha (39), kifungu kidogo cha kwanza (1), kinachompa mamlaka Mhe, Waziri anayehusika na masuala ya Umwagiliaji nchini, kwa kushauriana na Waziri wa Fedha, kuchapisha amri (Order) katika Gazeti la Serikali, akitamka Ada ya Huduma za Umwagiliaji na Ada nyingine zinazohusiana na shughuli za Uendeshaji na Matunzo katika maeneo ya umwagiliaji.

Katika kutekeleza kifungu hicho Mhe. Waziri wa Kilimo, baada ya kushauriana na Waziri wa Fedha, alitangaza katika Gazeti la Serikali namba (496P), la Tarehe 30/06/2021 na kutangaza amri inayojulikana kama ("The National Irrigation Service Fee" Order 2021), ambayo ilianza kutumika Tarehe 01 Julai 2021. Kwa amri hiyo (mkulima anatakiwa kulipa asilimia 5% ya Wastani wa mavuno kwa ekari kwa msimu), kwaajili ya kuendeleza huduma za umwagiliaji nchini.

Mtu yoyote atakaye kaidi kutekeleza amri hii anatenda kosa la jinai na baada ya kutiwa hatiani, atakabiliwa na adhabu ya kulipa faini ambayo sio chini ya Shilingi 1,000,000/= au kifungo cha mwaka mmoja au adhabu zote kwa Pamoja, (Kifungu cha 105 cha kanuni za Umwagiliaji).

**"Umwagiliaji - Kilimo Cha Uhakika"**